European Journal of
Linguistics
(EJL)

# Uchanganuzi Linganishi wa Usawiri wa Wahusika wa Kiume Katika Riwaya ya Kiswahili



CARI Journals

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025
www.carijournals.org

# Uchanganuzi Linganishi wa Usawiri wa Wahusika wa Kiume Katika Riwaya ya Kiswahili

[1*]Dorcas Kasiva Kimondiu,[2] Dr. Francis Musyoka [3] Dr. Esther Chomba

[1]Post Graduate Student: School of Humanities and Social Sciences South Eastern Kenya University

[2,3]Lecturer, School of Humanities and Social Sciences South Eastern Kenya University

*Accepted: 14st May, 2025, Received in Revised Form: 14st June, 2025, Published: 14st July, 2025*

**Ikisiri**

Makala haya yanakusudia kuchanganua na kulinganisha wahusika wa kiume katika riwaya teule za Kiswahili ambazo ni: *Mwisho wa Kosa,* (1987) iliyoandikwa na Zainabu Burhani, *Siku Njema* (1996), iliyoandikwa na Ken Walibora, *Taswira za Mawingu*, (2011) iliyoandikwa na Sinjiri Mukuba na *Nguu za Jadi,* (2021) iliyoandikwa na Clara Momanyi. Makala haya yanaegemea nadharia ya Mwanamume Mpya. Nadharia hii iliasisiwa na Beynon (2002). Nadharia ya Mwanamume Mpya inajaribu kueleza kwa nini baadhi ya wanaume hukaa na wake zao kwa usawa bila kuonesha tabia za mfumo dume ambazo huashiria kuwepo kwa taasubi ya kiume. Mihimili ya nadharia ya Mwanamume Mpya iliyoongoza makala haya ni kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii kujiendeleza kielimu na kikazi, kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia au watu wanaomzunguka, kutoonesha udikteta katika familia zao pamoja na jamii inayowazunguka, kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo na kukosoa nafsi zao na mazoea yao kama wanaume. Mbinu ya Fasihi Linganishi imetumika kulinganisha na kulinganua usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule. Data iliyotumika katika Makala haya ilitolewa maktabani. Maktabani, tasnifu, makala na vitabu vinavyohusiana na mada vilisomwa kwa kina. Uwasilishaji wa matokeo umefanyika kwa njia ya maelezo na michoro faafu. Matokeo yameonesha kuwa waandishi wa kike wamemsawiri mwanamume kwa mtazamo chanya ikilinganishwa na waandishi wa kiume. Kwa hivyo, kulingana na waandishi wa kike mwanamume ni mpya. Kulingana na mpito wa wakati waandishi wa karne ya ishirini wamemsawiri mhusika wa kiume kwa mitazamo chanya ikilinganishwa na waandishi wa karne ya ishirini na moja. Kwa hivyo mwanamume ni mpya kulingana na waandishi wa karne ya ishirini.

**Maneno Muhimu**: *Usawiri, Wahusika, Uchanganuzu, Ulinganishi, Mtazamo*

## 1. UTANGULIZI

Usawiri wa kijinsia umetafitiwa katika nyuga mbalimbali, kama vile elimu, ajira, malezi, afya, siasa, utamaduni, uchumi, fasihi na pia kwenye mitandao ya kijamii. Tangu kuanza kwa mawazo ya Ufeministi ulimwenguni, imekuwa ikijadiliwa ni namna gani wanawake wanaweza kujikomboa kutoka katika ufungwa wa mwanamume na kupata haki na wajibu sawa. Pamoja na hatua kubwa iliyopigwa, mapigano haya hayawezi kufanikiwa iwapo yatakuwa mapigano ya wanawake dhidi ya wanaume. Iwapo mwanamume ataachwa nyuma na asikombolewe kutoka katika ufungwa wa kifikra, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, mapambano haya hayatafanikiwa (Badru, 2019). Fasihi ina mchango mkubwa katika mapambano haya ya ukombozi wa mtoto wa kiume dhidi ya mfumo dume.

Makala haya yameangazia wahusika wa kiume katika riwaya teule za Kiswahili za waandishi wa kike na kiume. Riwaya za waandishi wa kike ni; *Mwisho wa Kosa* ya Zainabu Burhani na *Nguu za Jadi* ya Clara Momanyi. Riwaya za waandishi wa kiume ni; *Siku Njema* ya Ken Walibora na *Taswira za Mawingu* ya Sinjiri Mukuba. Wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi ili wawe sauti yake katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira (Muniu, 2011). Maoni yake yanashabihiana na ya Wamitila (2003) anayeeleza wahusika kama viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Wamitila (2008) anaibua hoja kuwa, maneno ya wahusika ni msingi mkubwa wa kuwakuza na kuwaendeleza hao hao wahusika. Kupitia kwa matendo na mazungumzo ya wahusika, wasomaji wanaweza kuzichanganua tabia zao.

Jamii mbalimbali zina mitazamo anuwai kuhusu wahusika wa kiume. Mwandishi hutokea katika jamii mahususi na kwa hivyo huweza kuwasuka wahusika wake kulingana na jamii alimokulia. Ken Walibora, Zainabu Burhani, Sinjiri Mukuba na Clara Momanyi ni wanajamii waliokulia katika jamii zao na tunaamini kuwa wamewasawiri wahusika wa kiume kwa mujibu wa jamii zao.Katika jamii kuna mjadala mkali unaotokana na suala la kijinsia. Kutokana na mitazamo kuwa mfumo dume unalenga kumkweza mwanamume na kumkandamiza mwanamke, tafiti na mijadala iliyofanyika imejigeza katika kuthamini namna ambavyo mfumo dume umekuwa chanzo cha unyanyasaji na utumwa kwa mwanamke. Tafiti nyingi zikiwemo za kijamii, kifasihi na kisheria zimechunguza nafasi ya mwanamke katika jamii na namna nafasi hiyo imeathiriwa na mfumo dume (Mrikau, 2015, Yego, 2013, Mosha, 2019, Ligaga, 2020). Wakati huo huo, haijazamiwa ni namna gani mfumo dume umekuwa chanzo cha utumwa kwa mwanamume ambaye ni sehemu ya jamii.

Jamii nyingi ulimwenguni zimekuwa zikidaiwa kumkweza mwanaume na kumdunisha mwanamke katika nyanja mbalimbali za maisha. Hata hivyo, baadhi ya tafiti za masuala ya kijinsia zinaonesha kuwa wapo wanaume ambao hukandamizwa na wanawake pamoja na mifumo inayowatawala (Mapunjo, 2014). Katika upande wa fasihi simulizi na fasihi andishi, jinsia ya kiume imekuwa ikijitokeza kwa namna ya kipekee kulingana na hitaji la jamii husika.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mikataba mbalimbali kuhusu usawa wa kijinsia kupitia mashirika mbalimbali. Kwa mfano shirika lisilo la kiserikali la *Center* for *Women and Children Development* (CWCD) nchini Tanzania limezidua mradi wa kuwatetea watoto wa kiume. Nzong'a, (2020) anaeleza kuwa ''kichwa'' kama jukumu la kimsingi la mwanaume kimetwaliwa na mwanamke. Kulingana na mtafiti huyu jamii humchukulia mwanamume kama kichwa cha familia. Kwa hivyo kama kichwa kimetwaliwa na mwanamke, ina maana kuwa mwanamume ametelekeza majukumu yake na kumwachia mwanamke. Anaelezea kuwa wanawake wamechukua jukumu la kuwa kichwa na kutoa amri na ushauri katika familia. Hii imebadilisha ukizano wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Kizazi cha sasa hakistahili kuadhibiwa kwa sababu ya ubaguzi uliosababishwa na mifumo ya jadi. Jinsia zote ya kike na ya kiume zina majukumu katika jamii kwa hivyo zote zinastahili kupiganiwa katika masuala ya kijamii. Ndungwa, (2012) anaeleza kuwa ufeministi kwa njia moja au nyingine umekuwa ukipigania haki za jinsia ya kike na kuinyanyasa ya kiume. Katika taifa la Kenya kumekuwa na tetesi kwamba baada ya miaka mingi ya kupigania usawa wa kijinsia, mtoto wa kike anatetewa sana na kumwacha nyuma mtoto wa kiume.

Jamii huchukulia kuwa mtoto wa kiume anajiweza na hivyo hahitaji kulindwa (Wizara ya Elimu, 2014). Suala hili likichukuliwa kwa uzito mtoto wa kiume ataangamia. Vilevile kule kumweka pembeni kunaweza kupelekea kujiingiza katika vitendo vya uhalifu. Wazo hili limetiliwa uzito na Hamisi, (2018) anapodai kuwa mtoto wa kiume asiposhughulikiwa ataathirika kama vifaru weupe barani Afrika. Jambo ambalo litampelekea kujiingiza katika kufanya vitendo vya uhalifu.Waandishi wamekuwa wakitazama mwelekeo wa jamii, itikadi, mila na desturi ili kuwasawiri wahusika wa kiume katika kazi zao (Kobia, 2008). Kwa mujibu wa Matundura na wenzake (2013) tajriba ya mtunzi wa jamii anayoiandikia huwa dira katika kuwafinyanga wahusika wake na kuwapa dhima kulingana na jinsia zao. Ingawa jinsia ya kiume imekuwepo katika jamii na kujitokeza katika kazi mbalimbali za

fasihi bado haijatafitiwa vya kutosha katika fasihi ya Kiswahili.

Makala haya yamedhamiria kuchanganua na kulinganisha usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili. Suala la mwanamke limetafitiwa na watafiti wengi. Katika harakati zao za kufanya utafiti wamechunguza masuala yanayoikumba jinsia ya kike. Hii inatokana na kuonekana kuwa ndiyo inayokabiliwa na matatizo na kukadamizwa (Mrikaria, 2015 na Noordin, 2017). Jinsia ni suala nyeti ambalo limewashughulisha wataalamu wengi katika jamii. Wasanii wa kike na wa kiume huwasawiri wahusika wao kwa njia tofauti (Mavisi, 2007 na Mnenuki, 2012). Kukosekana kwa tafiti nyingi za kutosha kuhusiana na jinsia ya kiume kumekuwa kukiathiri jamii kwa kuipa mtazamo kuwa jinsia ya kiume haikabiliwi na matatizo bali yenyewe ndiyo kisababishi cha matatizo kwa jinsia ya kike. Visa vya wavulana kujiunga na vikundi haramu vimekuwa vikiripotiwa mara kwa mara nchini Kenya. Kwa hivyo ni jukumu la jamii kusimama kidete na kuchunguza jinsia ya kiume inayozidi kupotea kila kuchao.

Momanyi, (2002) katika utafiti wa "Kiswahili na Masuala ya Uana" anadai kuwa mwanamume ndiye chanzo kikuu katika kumdunisha mwanamke katika sekta mbalimbali ndani ya jamii. Anadai kuwa mwanaume haoni kama kuna shida kwani maisha yanaendelea vizuri bila kujali masuala ya kijinsia. Utafiti huu wa Momanyi unaupa mwanga utafiti huu kwa kuwa unahusu wahusika wa kiume. Cha msingi ni kubaini kama kweli mwanamume ndiye chanzo cha dhuluma za mwanamke kama anavyodai Momanyi. Tofauti na utafiti wa Momanyi utafiti huu ulichunguza wahusika wa kiume katika riwaya teule za Kiswahili.Kanwa, (2022) katika utafiti wake wa shahada ya uzamifu ametafitia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Katika utafiti wake amebaini kuwa usawiri wa wahusika wa kiume na waandishi wanawake katika dhamira, taswira na mitazamo inayoibuliwa kuhusu wahusika wa kiume, uandishi wao haufanani. Wako ambao wanakuwa hasi zaidi na wengine chanya zaidi.

Kazi hii ilisaidia sana utafiti huu kwa kuwa imeibua taswira hasi na chanya katika kuwasawiri wahusika wa kiume. Uatafiti wa Kanwa (k.h.j) unaupa mwanga utafiti huu kwa kueleza kuwa wahusika wa kiume ni wa aina nzuri na mbaya katika matendo wayatendayo kwenye jamii zao.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025 www.carijournals.org

## 2. NADHARIA YA MWANAUME MPYA

Nadharia hii iliasisiwa na Beynon (2002) ambapo alifafanua kuwa mwanamume sio mbabe nyakati zote na kwa kila jamii bali wapo wanaume ambao wanajali sana, wasikivu na wanaotii maagizo ya kiuana. Kuna wanaume ambao muonekano ni wapole sana ila wanatawaliwa na mfumo dume. Kwa maana hiyo jamii ina wanaume mchanganyiko wakiwemo wanaume wapya yaani walioondokana na mfumo dume na ambao wanaushikilia. Nadharia hii inalenga kuwaonesha wanaume wapya ambao wamebadilika na kuwa katika utendaji mpya ikilinganishwa na mfumo uliotekelezwa na wanaume awali.

Mikondo mbalimbali ya uanaume inategemea elimu rasmi, vyombo vya mawasiliano na utamaduni wa Kimagharibi. Kwa mfano, wanaume wanaobadilika kuusheheni upya wa tabia wanakubali majukumu yoyote ya kiuana kwa kutojali jinsia, hawaonyeshi udikteta na wanawajibika katika kufanya majukumu ya kinyumbani. Pamoja na haya wanaweza kuzikosa nafasi zao na mazoea yao (Morell, 2002).Wanaume wapya huwasaidia wake zao kujiendeleza kielimu na kikazi. Vilevile, wanaweza kufanya kazi za jikoni kama kuosha vyombo na kulinda watoto bila kuogopa kuwa watafanyiwa masihara na wanaume wenzao au jamaa walioko karibu nao. Kulingana na Gill, (2003) mwanaume mpya ana hisia chanya, anawaheshimu wanawake na anawaona wanaume kwa wanawake kuwa viumbe sawa. Ni mtu anayejipenda kwa kuzingatia jinsi hulka yake ilivyo. Ana hisia za kike za kulinda watoto kama baba mwema. Nadharia hii inaungwa mkono na Newman, (2012) ambapo ameeleza kuhusu mtazamo huu mpya wa uana kuhusu mwanaume wa kisasa au anayetarajiwa kuwa wa kisasa kwa kumsaidia mkewe kama kiumbe sawa. Mkondo huu umesaidia kumchanganua mwanaume anayeelekea kuwa chanya kwa mwanamke tofauti na wanaume walio wengi katika jamii za Kenya na Afrika kama ilivyobainishwa na waandishi.

Mihimili ya nadharia hii imeainishwa na Beynon, (2002) kama ifuatavyo:

i) Kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii kujiendeleza kielimu na kikazi.

ii) Kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia au watu wanaomzunguka.

iii) Kutoonesha udikteta katika familia zao pamoja na jamii inayowazunguka.

iv) Kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na

kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo.

v) Kukosoa nafsi zao na mazoea yao kama wanaume

**2.1 Ulinganishaji Wa Namna Wahusika Wa Kiume Walivyosawiriwa Na Waandishi Wa Jinsia Ya Kike Na Kiume.**

Katika sehemu hii, Makala haya yameonesha namna waandishi wa jinsia tofauti walivyomsawiri mhusika wa kiume. Tumeorodhesha sifa zote za waandishi wa kila jinsia. Sifa zilizoibuliwa na waandishi wa kike (Zainabu Burhani na Clara Momanyi) zimejumulishwa pamoja. Vilevile, sifa zilizoibuliwa na waandishi wa kiume (Ken Walibora na Sinjiri Mukuba) zimejumulishwa pamoja. Sifa zinazofafana zimehesabiwa kama sifa moja katika kila kundi.

**2.2 Uainishaji Wa Sifa Za Mwanamume Katika Riwaya Za *Mwisho Wa Kosa* Na *Nguu Za Jadi.***

Katika sehemu hii, makala haya yameainisha sifa za wahusika wa kiume katika makundi mawili ili kuonesha idadi ya sifa chanya na sifa hasi kwa mujibu wa waandishi wa kike. Upande wa kushoto ni sifa chanya na upande wa kulia ni sifa hasi.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025
www.carijournals.org

**Jedwali 1: Sifa za mwanamume katika riwaya za *Mwisho wa Kosa* na *Nguu za Jadi*.**


| SIFA CHANYA | SIFA HASI |
|---|---|
| 1. Mwanamume kama mlezi mwema | 1 Mwanamume kama fisadi |
| 2. Mwanamume kama mshauri mwema | 2 Mwanamume kama kiongozi mbaya |
| 3. Mwanamume kama mwenye huruma | 3 Mwanamume kama mpendaraha na mlevi |
| 4. Mwanamume kama anayethamini jinsia ya kike | 4 Mwanamume kama katili |
| 5. Mwanamume kama mchapakazi na mwenye bidii | 5 Mwanamume kama mdanganyifu |
| 6. Mwanamume kama msomi | 6 Mwanamume kama asherati |
| 7. Mwanamume kama mkarimu na mwema | 7 Mwanamume kama mwenye hasira na hamaki |
| 8. Mwanamume kama mwenye utu | 8 Mwanamume kama mbabe |
| 9. Mwanamume kama mwaminifu | 9 Mwanamume kama kigeugeu na msaliti |
| 10. Mwanamume kama rafiki wa kweli | 10 Mwanamume kama mbinafsi |
| 11. Mwanamume kama jasiri | 11 Mwanamume kama kitega uchumi cha mwanamke |
| 12. Mwanamume kama msamehevu | |
| 13. Mwanamume kama mwenye msimamo madhubutu | |

Zainabu Burhani na Clara Momanyi ni waandishi wa kike. Uhakiki wa riwaya zao umeonesha kuwa wamewapa wahusika wa kiume jumla ya sifa ishirini na nne (24). Sifa chanya ni kumi na tatu (13) na sifa hasi ni kumi na moja (11) kama inavyooneshwa katika jedwali 1.

**Jedwali 2: Mitazamo ya wahusika wa kike kiasilimia.**

| Aina ya Usawiri | Idadi ya Sifa | Asilimia | Mitazamo |
|---|---|---|---|
| Usawiri Chanya | 13 | 54.2% | Mtazamo Chanya |
| Usawiri Hasi | 11 | 45.8% | Mtazamo Hasi |
| **Jumla** | **24** | **100%** | |

Takwimu hizi zimewakilishwa katika chati pai (1) ili kuonesha asilimia ya mitazamo kama ifuatavyo;




**Chati 1: Sifa chanya na hasi kwa mujibu wa waandishi wa kike**

Katika mchoro huu hapa juu, sifa chanya zinatawala kwa kuchukua asilimia hamsini na nne nukta mbili (54.2%) zikilinganishwa na asilimia arobaini na tano nukta nane (45.8%). Ni wazi kuwa waandishi hawa wa kike wamewasawiri wahusika wa kiume kwa mitazamo chanya. Hivyo basi, mwanamume ni mpya kulingana na nadharia ya Mwanmume Mpya

### 2.3 Uainishaji wa sifa za mwanamume katika riwaya za *Siku Njema* na *Taswaira za Mawingu.*

Katika sehemu hii, makala yameainisha sifa za wahusika wa kiume katika makundi mawili ili kuonesha idadi ya sifa chanya na hasi kwa mujibu wa waandishi wa kiume. Upande wa kushoto ni sifa chanya na kulia ni sifa hasi.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025



**Jedwali 3: Sifa za mwanamume katika riwaya ya *Siku Njema na Taswira za Mawingu.***

| SIFA CHANYA | SIFA HASI |
|---|---|
| 1. Mwanamume kama mshauri mwema | 1 Mwanamume kama mlipiza kisasi |
| 2. Mwanamume kama mwenye moyo safi | 2 Mwanamume kama kiumbe katili |
| 3. Mwanamume kama msiri | 3 Mwanamume kama kitega uchumi cha mwanamke |
| 4. Mwanamume kama mwenye mapenzi ya dhati | 4 Mwanamume kama mpendaraha na mlevi |
| 5. Mwanamume kama mwenye msimamo madhubuti | 5 Mwanamume kama mbakaji |
| 6. Mwanamume kama mwenye kuadilisha | 6 Mwanamume kama mwizi |
| 7. Mwanamume kama mtimiza ahadi | 7 Mwanamume kama mtamaduni |
| 8. Mwanamume kama mchapakazi na mwenye bidii | 8 Mwanamume kama mwenye kutamauka maishani |
| 9. Mwanamume kama mkarimu | 9 Mwanamume kama mbabe |
| 10. Mwanamume kama msomi | 10 Mwanamume kama mgomvi na mwenye hasira |
| 11. Mwanamume kama msamehevu | 11 Mwanamume kama asiyewajibika katika ndoa |
| 12. Mwanamume kama jasiri | 12 Mwanamume kama mbinafsi |
| 13. Mwanamume kama mvumilivu | 13 Mwanamume kama mdanganyifu |
| 14. Mwanamume kama mlezi mwema | 14 Mwanamume kama mvivu |
| 15. Mwanamume kama mwenye huruma | 15 Mwanamume kama asherati |
| 16. Mwanamume kama mwenye busara | 16 Mwanamume kama mbaguzi wa jinsia |


European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025
www.carijournals.org

Ken Walibora na Sinjiri Mukuba ni waandishi wa kiume. Uhakiki wa riwaya zao umeonesha kuwa wamewapa wahusika wa kiume jumla ya sifa thelathini na mbili (32). Sifa chanya ni kumi na sita (16) na sifa hasi ni kumi na sita (16) kama inavyooneshwa katika jedwali (3).

**Jedwali 4: Mitazamo ya mwandishi wa kiume kiasilimia**.

| **Aina ya Usawri** | **Idadi ya sifa** | **Asilimia** | **Mitazamo** |
|---|---|---|---|
| Usawiri Chanya | 16 | 50% | Mtazamo Chanya |
| Usawiri Hasi | 16 | 50% | Mtazamo Hasi |
| **Jumla** | **32** | **100%** | |

Takwimu hizi zimewakilishwa katika chati pai (2) ili kuonesha asilimia ya mitazamo kama ifuatayo:




**Chati 2: Sifa chanya na hasi kwa mujibu wa waandishi wa kiume.**

Katika mchoro huu hapa juu, sifa chanya na hasi zimelingana kwa asilimia hamsini kila moja (50%). Ni dhahiri kuwa waandishi wa kiume wana mitazamo sawa kwa wahusika wa kiume. Kwao wahusika wanaume si chanya wala hasi.

## 3.0 ULINGANISHAJI WA MITAZAMO YA WAANDISHI WA RIWAYA YA KISWAHILI KWA MUJIBU WA MPITO WA WAKATI (KARNE YA ISHIRINI NA KARNE YA ISHIRINI NA MOJA).

Katika sehemu hii, mtafiti ameonesha namna waandishi wa karne tofauti walivyowasawiri wahusika wa kiume. Kwanza, sifa zote za waandishi wa karne ya ishirini zimedondolewa na kujumuliswa pamoja. Sifa zinazofanana zimehesabiwa kama sifa moja. Pili, sifa zote za waandishi wa karne ya ishirini na moja zimedondolewa na kujumulishwa pamoja. Vilevile, sifa zinazofanana zimehesabiwa kama sifa moja.

### 3.1 Uainishaji Wa Sifa Za Mwanamume Katika Riwaya Za *Mwisho Wa Kosa* Na *Siku Njema.*

Katika sehemu hii, mtafiti ameainisha sifa za wahusika wa kiume katika makundi mawili kama inavyodhihirika katika jedwali (4.13) ili kuonesha idadi ya sifa chanya na sifa hasi kwa mujibu wa waandishi wa karne ya ishirini. Upande wa kushoto ni sifa chanya na upande wa kulia ni sifa hasi.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025
www.carijournals.org

**Jedwali 5: Sifa za mwanamume katika riwaya za *Mwisho wa Kosa* na *Siku* Njema.**


| SIFA CHANYA | SIFA HASI |
|---|---|
| 1. Mwanamume kama mlezi mwema | 1. Mwanamume kama fisadi |
| 2. Mwanamume kama mshauri mwema | 2. Mwanamume kama kiongozi mbaya |
| 3. Mwanamume kama mwenye huruma | 3. Mwanamume kama mpendaraha na mlevi |
| 4. Mwanamume kama mwenye kuthamini jinsia ya kike | 4. Mwanamume kama katili |
| 5. Mwanamume kama mchapakazi na mwenye bidii | 5. Mwanamume kama mdanganyifu |
| 6. Mwanamume kama msomi | 6. Mwanamume kama asherati |
| 7. Mwanamume kama mkarimu na mwema | 7. Mwanamume kama mwenye hasira na hamaki |
| 8. Mwanamume kama mwenye utu | 8. Mwanamume kama mbabe |
| 9. Mwanamume kama mwaminifu | 9. Mwanamume kama mlipiza kisasi |
| 10. Mwanamume kama rafiki wa kweli | 10. Mwanamume kama kitega uchumi cha mwanamke |
| 11. Mwanamume kama mwenye moyo safi | 11. Mwanamume kama mbakaji |
| 12. Mwanamume kama msiri | 12. Mwanamume kama mwizi |
| 13. Mwanamume kama mwenye mapenzi ya dhati | 13. Mwanamume kama mtamaduni |
| 14. Mwanamume kama mwenye msimamo madhubuti | 14. Mwanamume kama mwenye kutamauka maishani |
| 15. Mwanamume kama mtimiza ahadi | |
| 16. Mwanamume kama mkarimu | |
| 17. Mwanamume kama mwenye kuadilisha | |
| 18. Mwanamume kama msamehevu | |

Zainabu Burhani na Ken walibora ni waandishi wa kike na kiume mtawalia. Waliandika riwaya zao katika kipindi cha karne ya ishirini. Riwaya hizi ni *Mwisho wa Kosa,* (1987) na *Siku Njema,* (1996). Uhakiki wa riwaya zao umeonesha kuwa wamewapa wahusika wa kiume jumla ya sifa thelathini na mbili (32). Sifa chanya ni kumi na nane (18) na sifa hasi ni kumi na nne (14) kama inavyooneshwa na jedwali (4.13) hapo juu.

**Jedwali 6: Mitazamo ya waandishi wa karne ya ishirini kiasilimia.**

| Aina ya Usawiri | Idadi ya Sifa | Asilimia | Mitazamo |
|---|---|---|---|
| Usawiri Chanya | 18 | 56.3% | Mtazamo Chanya |
| Usawiri Hasi | 14 | 43.7% | Mtazamo Hasi |
| **Jumla** | **32** | **100%** | |

Takwimu hizi zimewakilishwa katika chati pai 4 ili kuonesha asilimia ya mitazamo kama ifuatavyo:




**Chati 3: Sifa chanya na hasi kwa mujibu wa waandishi wa karne ya ishirini.**

Katika mchoro huu hapo juu, sifa chanya zinatawala kwa kuchukua asilimia hamsini na sita nukta tatu (56.3%) zikilinganishwa na sifa hasi ambazo zinachangia kwa asilimia arobaini na tatu nukta saba (43.7%). Ni bayana kuwa waandishi hawa wa karne ya ishirini wamewasawiri wahusika wa kiume kwa mitazamo chanya. Kwa hivyo, kulingana na

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025


nadharia ya Mwanamume Mpya, kwao mwanamume wa karne ya ishirini ni mpya kupitia sifa chanya walizompa.

### 3.2 Uainishaji Wa Sifa Za Mwanamume Katika Riwaya Za *Taswira Za Mawingu* Na *Nguu Za Jadi.*

Katika sehemu hii, makala yameainisha sifa za wahusika wa kiume katika makundi mawili. Makundi haya yamedhihirishwa na jedwali (7) ili kuonesha idadi ya sifa chanya na sifa hasi kwa mujibu wa waandishi wa karne ya ishirini na moja. Upande wa kushoto ni sifa chanya na upande wa kulia ni sifa hasi.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 49 - 67, 2025
www.carijournals.org

**Jedwali 7: Sifa za mwanamume katika riwaya za *Taswira ya Mawingu* na *Nguu za Jadi.***


| SIFA CHANYA | SIFA HASI |
|---|---|
| 1. Mwanamume kama mlezi mwema | 1. Mwanamume kama mpendaraha na mlevi |
| 2. Mwanamume kama mchapakazi na mwenye bidii | 2. Mwanamume kama mbabe |
| 3. Mwanamume kama jasiri | 3. Mwanamume kama mgomvi na mwenye hasira |
| 4. Mwanamume kama mvumilivu | 4. Mwanamume kama asiyewajibika katika ndoa |
| 5. Mwanamume kama msomi | 5. Mwanamume kama mbinafsi |
| 6. Mwanamume kama mshauri mwema | 6. Mwanamume kama mbakaji |
| 7. Mwanamume kama mwenye huruma | 7. Mwanamume kama mwizi |
| 8. Mwanamume kama mwenye mapenzi ya kweli | 8. Mwanamume kama mdanganyifu |
| 9. Mwanamume kama msamehevu | 9. Mwanamume kama mvivu |
| 10. Mwanamume kama mwenye busara | 10. Mwanamume kama mwenye uchu wa mwanamke |
| 11. Mwanamume kama mwenye msimamo madhubuti | 11. Mwanamume kama mbaguzi wa kijinsia |
| 12. Mwanamume kama mwenye kuthamini jinsia ya kike | 12. Mwanamume kama fisadi |
| | 13. Mwanamume kama asherati |
| | 14. Mwanamume kama kiongozi mbaya |
| | 15. Mwanamume kama mbinafsi |
| | 16. Mwanamume kama katili |
| | 17. Mwanamume kama kitega uchumi cha mwanamke |

Sinjiri Mukuba na Clara Momanyi ni waandishi wa kike na kiume mtawalia. Waliandika riwaya zao katika kipindi cha karne ya ishirini na moja. Riwaya hizi ni *Taswira za Mawingu*, (2011) na *Nguu za Jadi*, (2021). Uhakiki wa riwaya hizi umeonesha kuwa wamewapa wahusika wa kiume jumla ya sifa ishirini na tisa (29). Sifa chanya ni kumi na mbili (12) na sifa hasi ni kumi na saba (17) kama inavyooneshwa na jedwali (7) hapo juu.

**Jedwali 8: Mitazamo ya waandishi wa karne ya ishirini na moja kiasilimia.**

| Aina ya Usawiri | Idadi ya Sifa | Asilimia | Mitazamo |
|---|---|---|---|
| Usawiri Chanya | 12 | 41.4% | Mtazamo Chanya |
| Usawiri Hasi | 17 | 58.6% | Mtazamo Hasi |
| **Jumla** | **29** | **100%** | |

Takwimu hizi zimewakilishwa katika chati pai (4) ili kuonesha asilimia ya mitazamo kama ifuatavyo.




**Chati 4: Mitazamo chanya na hasi kwa mujbu wa waandishi ya karne ya ishirini na moja.**

Katika mchoro huu hapo juu, sifa hasi zinatawala kwa kuchukua asilimia hamsini na nane nukta sita (58.6%) zikilinganishwa na sifa chanya ambazo zinachangia kwa asilimia arobaini na moja nukta nne (41.4%). Hili ni dhibitisho kuwa waandishi hawa wa karne ya ishirini na moja wamewasawiri wahusika wa kiume kwa mitazamo hasi. Kulingana nao, mwanamume bado si mpya.

## 4.0 KIWANGO CHA KUFANANA NA KUTOFAUTIANA KWA WAANDISHI WA KIKE NA KIUME.

Kutofautiana na kufanana kwa waandishi kunaonesha kiwango cha uhusiano wa kimtazamo. Kutokana na uchambuzi wa data, ni wazi kuwa waandishi wa kike wana mtazamo chanya kuhusu wahusika wa kiume. Hii imebainishwa na kiwango cha asilimia. Mtazamo chanya umebainishwa kwa kiwango cha asilimia hamsini na nne nukta mbili (54.2%) huku mtazamo hasi ukibainishwa kwa asilimia arobaini na tano nukta nane (45.8%). Kulingana na waandishi wa kike mwanamume ni mpya. Katika kiwango cha kutofautiana kimtazamo, waandishi wa kiume wana mitazamo sawa kuhusu wahusika wa kiume. Hii inabainishwa na kiwango cha asilimia. Mitazamo yote miwili, hasi na chanya imelingana kwa asilimia hamsini (50%). Kulingana na waandishi hawa wa kiume mwanamume kwao ni sawa si mpya wala si mkale.

Kulingana na mpito wa wakati; yaani karne ya ishirini (20) na karne ya ishirini na moja (21). Waandishi wa karne ya ishirini wana mtazamo chanya kuhusu mhusika wa kiume. Hii inabainishwa kwa kiwangpo cha asilimia. Katika mtazamo chanya, waandishi hawa wamedhihirisha kiwango cha asilimia hamsini na sita nukta tatu (56.3%) ikilinganishwa na asilimia arobaini na tatu nukta saba (43.7%) ambao ni mtazamo hasi. Kulingana na waandishi hawa mwanamume ni mpya, kwani wana mtazamo chanya kuhusu wahusika wa kiume.Waandishi wa karne ya ishirini na moja wana mtazamo hasi kuhusu wahusika wa kiume. Hii inadhihirishwa na kiwango cha asilimia. Mtazamo hasi unatawala kwa asilimia hamsini na nane nukta sita (58,6%) nao mtazamo chanya ukichangia asilimia arobaini na moja nukta nne (41.4%). Hii ni idhibati kuwa waandishi wa karne ya ishirini na moja wana mtazamo hasi kuhusu wahusika wa kiume. Kwa hivyo, mwanamume si mpya kulingana na waandishi hawa.

## 5.0 HITIMISHO

Katika Makala haya tulichanganua na kulinganisha usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya Kiswahili. Makala yamethibitisha kuwa kuna baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume ambao ni wapya. Wahusika hawa wamesawiriwa kwa njia chanya. Wanaume hao huonesha matendo mema wanayotenda kwao na kwa wanajamii wengine. Wamesawiriwa kama walezi wema, washauri wema, wenye huruma, wenye kuthamini jinsia ya kike, wenye bidii, wasomi, wakarimu, wenye mapenzi ya dhati miongoni mwa sifa nyingine

chanya. Aidha, kuna wale waliosawiriwa kwa mitazamo hasi. Wamesawiriwa kama viongozi wabaya, wadanganyifu, katili, wenye hasira, fisadi, wapenda raha, walevi, asherati miongoni mwa sifa nyingine hasi.

Katika kiwango cha ulinganishaji, waandishi wa kike kwa pamoja wana mitazamo chanya kuhusu mhusika wa kiume. Kulingana nao, mwanamume ni mpya kwa sababu wamempa mhusika wa kiume idadi kubwa ya sifa chanya. Kwa upande wa waandishi wa kiume, imebainika kuwa sifa zote zikijumulishwa pamoja, wana mitazamo sawa wa mhusika wa kiume. Katika ulinganishaji wa mpito wa wakati, waandishi wa karne ya ishirini wamemsawiri mwanamume kwa sifa chanya ikilinganishwa na kipindi cha karne ya ishirini na moja. Wingi wa sifa chanya unaashiria upya huu. Kulingana na waandishi wa karne ya ishirini na moja, bado mwanamume si mpya. Wingi wa sifa hasi unaashiria ukale wa mwanamume.

**MAREJELEO**

Badru, Z. (2019). "Mfumo Dume- Chanzo cha Ufungwa wa Mwanamume: Uhakiki wa Semi Kutoka Jamii za Kiafrika." Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Haijachapishwa*)

Beynon, J. (2002). Masculinity and Culture. Philadelphia, Open University Press. Bly, R. (1990). *Iron John: A Book about Men.* New York: Minesota Publishers Ltd.

Burhani, Z. (1987). *Mwisho wa Kosa*. Nairobi: Longhorn Kenya

Hamisi, L. (2018). The Boy Child and New Gender Imperatives in Kenya: Investigating School Dropout among Boys in Marakwet County.

Kobia, J. (2008). "Taswira za Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume Miongoni mwa Waigembe." *Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu katika Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (*Haijachapishwa*).

Ligaga, D. (2020). *Women, Visibility and Morality in Kenyan Popular Media.* Grahamstown: NISC (pty) Ltd.

Matandura, B. (2007). "Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto" M.A Thesis University of Nairobi

Mapunjo, G. (2014). "Usawiri wa Mwanamke kama Kiongozi katika Tamthiliya: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (*Haijachapishwa*)

Ministry of Education, Science and Technology, (2014). Free Secondary Education Policy in Kenya.

Mirikau, S. (2011). "Tasnifu ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila" *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili* Chuo Kikuu cha Nairobi.

Momanyi, C. (2021). *Nguu za Jadi.* Nairobi vide-muwa

Morell, R. (2002). "Mutations in a Novel Genre Are Associated with Hearing Loss, Linked to the DFNB 6. Locus vol.7

Mosha, D. (2019). Ulinganishaji wa Majukumu ya Wahusika Kijinsia katika Nyimbo za Watoto na Uhalisia Wake katika Malezi ya Watoto Nchini Tanzania. *Tasnifu ya Uzamivu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*Haijachapishwa*).

Mukuba, S. (2011). Taswira za Mawingu. Nairobi: Moran Publishers

Muniu, G. (2011). *Ujagina wa Mwanamke katika Pango.* Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ndungwa, B. (2012). "The Challenges of Akamba Single Mothers in References to Parenting the Boy Child in the Light of Chistian Complementary Feminism." M.A Thesis University of Nairobi.

Newman, M. (2012). Community Food Webs Data and Theoty, USA, *International Union for Conservation of Nature*, University of Arizona.

Nzong'a, P. (2020)." Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume katika Hadithi Fupi za Kiswahili" *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Yego, E. (2013). "Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Anavyotetewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar" *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili* Chuo Kikuu cha Nairobi. (*Haijachapisha*)

©2025 by the Authors. This Article is an open access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/)